compass
The Salvation Army's Global Strategic Framework

# Mazungumzo ya Compass




*Tunawawezesha watu wetu namna gani waongoze, wajifunze na wakue? Je, mipango na miradi yetu inaendana na utume wetu? Tunafanya nini leo ambacho kitagusa siku zetu zijazo? Nguvu zetu ni zipi na tunahitaji kukua katika maeneo yapi?*

Karibu kwenye *Mazungumzo ya Compass*! *Mazungumzo ya Compass* yameandaliwa kukusaidia uone uko wapi; kukusaidia uweke vipaumbele vyako na uungane na Mungu na watu wake kwa kina. Maswali katika maandishi haya yametengenezwa kuwa kama mahali pa kuanzia ili kukusaidia uungane na Mfumo wa Kazi wa Mkakati wa Dunia (Global Strategic Framework), pale ulipo. Compass ni kwa kila mmoja! Jenerali Lyndon Buckingham anamtaka kila mmoja anayehusika na Jeshi ashiriki – kuuliza maswali na kuwa sehemu ya majibu.

## Compass ni nini?

Compass ni jina la Mfumo wa Kazi wa Mkakati wa Jeshi Duniani. Ni mpango wa duniani kote wa kuelekeza njia ya kwenda mbele wakati Jeshi linapoendelea kukabiliana na mahitaji ya wanadamu kwa jina Lake. Compass siyo mpango, wala haiji kuwa mbadala wa mpango mkakati wenu au mchakato wenu wa uhakiki. Ni mpangilio wa vipaumbele vilivyoandaliwa kutusaidia tuangalie maisha na afya ya chombo chetu na tutafute njia ya kwenda mbele. Compass inazingatia maeneo matatu kwa ujumla: kuwawezesha watu, kuimarisha mguso wa utume, na kuanzisha urithi unaodumu.




**Unaweza kupata habari zaidi kuhusu Compass hapa:**
sar.my/strategy

# WATU

### Maisha ya Kiroho

Lengo: Kuimarisha kina cha kiroho na kujitoa kwa utakatifu kati ya waumini wote wa Jeshi la Wokovu na wabakie wa kweli kwa maadili ya utume wetu kama Jeshi la Wokovu.

- Tunamfahamu Yesu vizuri namna gani? Je, maisha yetu ya kiroho yanakua kama kanisa na kama watu binafsi?
- Biblia ina umuhimu gani kwangu? Je, ni kipaumbele kikaoni?
- Tunafanya nini kuwasaidia watu wamfahamu Yesu vizuri zaidi?
- Tunafahamu utakatifu kuwa ni nini?
- Karama zangu za rohoni ni zipi? Nazitumia namna gani kutimiza makusudi ya Mungu?

### Maendeleo ya Kiongozi

Lengo: Kuwaendeleza maafisa na viongozi wa huduma wanaoonyesha utumishi wa kweli, na ambao kiroho wamekomaa, wenye uwezo na waliowezeshwa kwa ajili ya majukumu yao ya sasa na yale yajayo.

- Fikiria kuhusu kiongozi wa kipekee uliyemfahamu – nini kilimfanya awe wa kipekee?
- Tunaweza kufanya nini kuwahimiza watu wengi wachukue wajibu wa uongozi?

### Ustawi wa Afisa

Lengo: Kuanzisha mwelekeo wa jumla kwa ustawi wa afisa, tukizingatia afya ya kimwili, kiakili na kiroho pamoja na kutoa mazingira yanayostahili ya kuishi.

- Je, maafisa wetu wanastawi? Tunafanya nini kuwatia moyo na kuwasaidia?
- Kwa kufahamu kwamba maafisa wengi duniani hawapokei riziki kamili na/au wanaishi katika mazingira duni, je, tuna lolote tunaloweza kufanya ili kuwasaidia?
- Tunawezaje kuwahimiza watu wafikirie kuhusu uafisa wa Jeshi la Wokovu?

compass
The Salvation Army's Global Strategic Framework



## UTUME

### Uanachama

Lengo: Kuanzisha uwazi na usahihi wa kuelezea jinsi watu wanavyokuwa sehemu ya ushirika wa Jeshi la Wokovu.

- Maana yake nini kuwa 'sehemu ya' ndani ya Jeshi la Wokovu?
- Unajengaje mahusiano ndani ya kikao/ushirika wetu?
- Tunaweza kufanya nini kuwatia moyo watu waungane na kikao/ushirika wetu?

### Mjumuisho wa Utume

Lengo: Kuanzisha kanuni za kikao na ushirika zitakazo jumuisha utume na kuwezesha ukuaji wa waumini.

- Tunafahamu utume wetu vizuri namna gani na tuna wajibu gani ndani yake?
- Tumeungana vizuri namna gani na mipango mingine ya Jeshi la Wokovu iliyo jirani nasi?
- Tunawezaje kuunganisha kikamilifu zaidi familia ya kikao chetu na watu walio katika jamii yetu?
- Nawezaje kuwatumikia watu wengine? Nachangia namna gani kwenye utume na huduma ya Jeshi?

### Agano

Lengo: Kuhakiki Agano la Askari na lile la Afisa ili kuthibitisha kufaa kwake  katika Jeshi la Wokovu la karne ya 21.

- 'Agano' maana yake nini?
- Jukumu la Maagano ya Askari na Rafiki ni lipi?

## URITHI

### Mgawanyo wa Rasilimali

'Ufanisi wa Utume' unaelezwa kuwa ni kiwango ambacho mpango au sera huimarisha utume wa Jeshi la Wokovu. Hutusaidia vizuri namna gani tuhubiri habari njema ya Yesu Kristo na kukabiliana na mahitaji ya wanadamu katika jina lake?

- Tunafanya nini sasa ambacho kitakuwa na matokeo ya muda mrefu?
- Je, kuna mipango au shughuli ambazo tumezing'ang'ania, lakini hazitumikii tena kusudi?
- Je, tunawekeza rasilimali zetu (watu, fedha, muda, nafasi) kwa usahihi?

### Maswali machache ya mwisho:

*Wakati wa mazungumzo haya, Mungu amesema nini na wewe?*
*Mungu amekupa utambuzi au mwongozo gani?*
*Utachukua hatua gani kuhusu yale ambayo Mungu anasema?*